



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Kumb. Na. JB.201/307/21/08

23/02/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA
ANWANI ZA MAKAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anapenda kuwatangazia Watanzania wenye Sifa **nafasi 100 za Ajira ya muda** kwa kazi ya kukusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Vitongoji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

1. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea.
- ii. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 40.
- iii. Awe anamiliki simu janja ya "android" yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa muda wa siku nzima na uwezo wa kupokea Mfumo wa Anwani za Makazi.
- iv. Awe na barua pepe (email address) inayofanya kazi.
- v. Awe ni mkazi wa Kata/Kijiji/Kitongoji husika.

2. MAJUKUMU

- i. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma za jamii.
- iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba na wapangaji na kuziingiza/kutuma kwenye mfumo wa **NaPA**.
- iv. Kutuma Data kwenye mfumo wa Anwani za Makazi wa Halmshauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

3. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA VIELELEZO VIFUATAVYO:

- i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- ii. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- iii. Picha 2 ndogo (passport size).

4. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za Maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya Mwombaji, Namba ya Simu, Barua Pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Nyang'hwale kupitia kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata husika, kabla au ifikapo tarehe 28/02/2022 saa 9:30 Alasiri kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W),

S.L.P 352,

NYANG'HWALE

N.B: Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale kupitia www.nyanghwaledc.go.tz


Rajabu Mmunda

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

NYANG'HWALE.

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 352
NYANG'HWALE.**